***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.***

Mwaka __1__ ulipoanza, sote tulifurahia kurudi katika shule __2__. Shule hiyo inajulikana na watu __3__ hapa kijijini. Ina wanafunzi wengi na pia mabasi __4__. Mabasi yote ya shule hiyo yamepakwa rangi ya __5__. Tulipowasili shuleni, tuliingia madarasani na kuketi kwenye viti __6__. Mwalimu __7__ ambaye tulimpenda sana aliingia darasani na kutuamkua, "__8__ wanafunzi?" Sote tulimjibu kwa heshima na __9__. Kengele __10__ tulielekea gwarideni. Tulisimama kwa safu na kuimba wimbo __11__ taifa. Baadaye walimu walitukagua iwapo __12__ zetu zilikuwa safi. Mwalimu mkuu alitushauri kuwa tuwe tukinywa maji __13__ ili tuepuke magonjwa kama __14__. Alipomaliza tulimpigia __15__ halafu tukaenda madarasani.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. haya | B. hizi | C. hii | D. huu |
| 2. | A. letu | B. kwetu | C. mwetu | D. yetu |
| 3. | A. wote | B. wowote | C. sote | D. yote |
| 4. | A. wengi | B. mingi | C. mengi | D. nyingi |
| 5. | A. buluu | B. manjano | C. kijani | D. hudhurungi |
| 6. | A. vyetu | B. zetu | C. chetu | D. yetu |
| 7. | A. huo | B. moja | C. mmoja | D. wawili |
| 8. | A. shikamoo | B. masalheri | C. hamjambo | D. kwaherini |
| 9. | A. adhabu | B. adabu | C. adhahabu | D. nidhabu |
| 10. | A. ilipokirizwa | B. alipolia | C. kilipokirizwa | D. alipotuita |
| 11. | A. ya | B. wa | C. za | D. la |
| 12. | A. jezi | B. nguo | C. mavazi | D. sare |
| 13. | A. mengi | B. masafi | C. msafi | D. safi |
| 14. | A. kifaduro | B. UKIMWI | C. kipindupindu | D. kifuakikuu |
| 15. | A. makofi | B. magoti | C. makelele | D. kofi |

***Kuanzia nambari 16 mpaka 30, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.***

**16.** Rangi ya juu kabisa ya upinde wa mvua huwa gani?

A. Nili
B. Machunga
C. Urujuani
D. Nyekundu

**17.** Jaza nafasi ukitumia kiulizi sahihi.

**Mwalimu anataka kabati ________?**

A. lipi    B. ipi
C. kipi    D. upi

**18.** Chagua sentensi iliyo katika wakati uliopita.

A. Nimeinawa mikono vizuri.
B. Tutaenda sokoni na mama.
C. Wanafunzi waliandika insha.
D. Anajua kusoma gazeti.

19. Kamilisha methali:
**Haraka haraka haina ______**
A. mwendo B. baraka
C. kufika D. kuchelewa

20. Jibu gani linaloonyesha wingi wa;
**Daktari huyu alimdunga mgonjwa sindano.**
A. Daktari hawa waliwadunga wagonjwa sindano.
B. Madaktari hawa waliwadunga wagonjwa sindano.
C. Daktari hawa waliwadunga wagonjwa masindano.
D. Madaktari hawa walimdunga wagonjwa sindano.


21. Tambua nafsi katika sentensi hii.
**Mtoto huyu akimaliza kufanya kazi atakupa wewe.**
A. huyu B. kufanya
C. wewe D. kazi

22. Shairi lenye mishororo mitano katika kila ubeti huitwaje?
A. malenga B. takhmisa
C. kibwagizo D. tarbia

23. Chagua sentensi iliyoakifishwa vizuri.
A. mji mkuu wa Kenya ni Nairobi.
B. Je! Jina lako ni nani?
C. Kwa nini utatembea polepole?
D. Alinunua, maembe, ndizi na unga.

24. **'Kipofu, kipepeo, chawa'** ni maneno yanayopatikana katika ngeli ya:
A. KI - VI B. A - WA
C. U - I D. LI - YA

25. Sehemu gani ya mchoro ambayo imepakwa rangi?




A. Robo B. Nusu
C. Robo tatu D. Thuluthi

26. Kanusha: **Njoo hapa**
A. Usinjoo hapa B. Usije hapa
C. Sitanjoo hapa D. Siji hapa

27. Jaza nafasi ukitumia kiashiria.
**Mbuzi ______ amekunywa maji.**
A. huyu B. wangu
C. mzuri D. mmoja

28. Vifaa hivi hutumika kufanya nini?



A. Kukunia nazi.
B. Kunywea maji.
C. Kupakulia chakula.
D. Kupondea au kutwangia nafaka.

29. Chagua orodha yenye vimilikishi pekee.
A. Juu ya, chini ya, mbele ya.
B. Wangu, wake, wao.
C. Lipi, upi, gani.
D. Kimoja, mbili, wengi.

30. Jaza pengo ukitumia kiunganishi kinachofaa.
**Mtoto amefurahi ______ ameshiba.**
A. lakini B. wala
C. ingawa D. kwa sababu

***<u>Soma barua ifuatayo kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.</u>***

SHULE YA BUSARA,
S.L.P. 231,
BOMBOLULU.
7:1:2020.

Kwa rafiki Neema,

Pokea salamu tele kutoka kwangu hapa nilipo. Unaendeleaje huko uliko? Habari za shule yako mpya? Sisi huku nyumbani tu wazima. Nimefurahia sana kujiunga na darasa la tano.

Lengo la kukuandikia barua hii ni kukueleza jinsi nilivyosherehekea sikukuu ya mwaka mpya na pia kukuambia mambo niliyoyafanya wakati wa likizo. Likizo ya Disemba ilikuwa na shughuli nyingi. Jambo la kwanza, nilienda kumtembelea nyanya yangu kule Laikipia. Safari ya kutoka Mombasa hadi Laikipia ilikuwa ndefu mno. Baba alinibeba kwa gari lake kutoka Bombolulu hadi mjini Mombasa. Nilitumia gari la moshi kusafiri hadi Nairobi kisha shangazi yangu akanisaidia kuabiri matwana iliyonipeleka hadi Laikipia. Nilikaa na nyanya kwa muda wa wiki mbili nikimsaidia kufanya kazi za hapa na pale. Baada ya wiki hizo mbili, baba alikuja kumjulia nyanya hali kisha akarudi na mimi huko nyumbani.

Nilipowasili kwetu, nilijiunga na vijana wenzangu wa pale tunapoishi ili kuwatembelea mayatima. Tulikusanya vitu muhimu kama vile vyakula, nguo, viatu, vyandarua na vitu vingine muhimu. Pia tuliwaomba wazazi wetu na walezi pesa ambazo tulizikusanya na kuwapelekea. Tulienda katika makao ya mayatima ya Tumaini. Watoto hao walifurahia sana kucheza pamoja na sisi. Pia tulikula pamoja halafu tukaimba na kumsifu Mungu.

Siku ya Krismasi, tulienda kanisani kufurahia na kusherehekea. Tulikula pamoja na majirani, tulicheza na kuimba pamoja. Pia tulienda Kanisani tarehe moja, Januari ili kufurahia na kumshukuru Mungu kwa kutuwezesha kuuona mwaka mpya. Ningependa kukomea hapo kwa sababu muda wangu umemalizika. Nitakutembelea shule zikifungwa mwezi wa nne. Kila la heri.

Ni mimi rafiki yako,
Salma Tegemeo.

31. Barua hii ni ya aina gani?
A. Kirafiki B. Kiofisi
C. Rasmi D. Kujuana

32. Mwandishi wa barua hii anaishi wapi?
A. Laikipia B. Nairobi
C. Bombolulu D. Mjini

33. Mwaka uliopita, mwandishi wa barua hii alikuwa katika darasa lipi?
A. 3 B. 4
C. 5 D. 6

34. Lengo la mwandishi kuandika barua hii ni gani?
A. Kumweleza rafiki anavyoendelea shuleni.
B. Kumsalimia rafiki yake.
C. Kuelezea alivyosherehekea sikukuu ya Jamhuri.
D. Kumweleza rafiki yake mambo aliyoyafanya wakati wa likizo.

35. Nyanya wa mwandishi wa barua hii alikuwa akiishi wapi?
A. Laikipia B. Nairobi
C. Bombolulu D. Mombasa

36. Kulingana na aya ya pili, ni kweli kuwa:
A. mwandishi alitumia gari la moshi kusafiri kutoka Bombolulu hadi Nairobi.
B. mwandishi alienda Laikipia akiwa na dada yake.
C. mwandishi aliishi na nyanya yake kwa muda wa mwezi mmoja
D. mwandishi alirudishwa nyumbani kwao na baba yake.

37. Barua hii iliandikwa muhula gani?
A. 1 B. 2
C. 3 D. 4

38. Ni nini ambacho mwandishi wa barua alifanya pamoja na vijana wenzake?
A. Kuenda shuleni.
B. Kumtembelea nyanya.
C. Kuwatembelea mayatima.
D. Kusherehekea siku ya Krismasi.

39. Mwandishi wa barua hii ni nani?
A. Busara B. Salma Tegemeo
C. Neema D. Neema Salma

40. Katika aya ya mwisho, kwa nini mwandishi na wenzake walimshukuru Mungu?
A. Kwa kuwapa safari njema.
B. Kwa kuwapa sherehe nzuri ya Krismasi.
C. Kwa kuwawezesha kuuona mwaka mpya.
D. Kwa kuwapa afya njema.

**Soma kwa makini habari ifuatayo kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.**

Mnyama nimpendaye ni ng'ombe. Ng'ombe ni mnyama anayefugwa nyumbani ambaye ana pembe, miguu minne na nundu. Hata hivyo, kunao ng'ombe ambao hawana nundu wala pembe. Ng'ombe wa kiume ambaye amekomaa anaitwa fahali, yule wa kike anaitwa mbuguma. Ng'ombe ana faida nyingi sana katika maisha yetu. Jambo la kwanza, ng'ombe hutupa chakula. Chakula ambacho hutokana na ng'ombe ni nyama na maziwa. Nyama huweza kuliwa pamoja na ugali, wali au chapati. Maziwa nayo huweza kutumika kupikia chai, uji, kuongezwa katika mboga au kunywewa moja kwa moja. Nyama na maziwa hujenga mwili wa yule anayetumia. Mifupa na nyama ya ng'ombe huweza kutokoswa na kuunda mchuzi ambao huongeza nguvu kwenye mifupa.

Ngozi ya ng'ombe hutumika kuundia vitu mbalimbali. Vitu hivyo ni kama vile mikoba, viatu na mishipi au mikanda. Kwato na pembe pia huweza kutumika kutengeneza gundi na chaki. Ng'ombe huweza kula nyasi, majani na vyakula vinavyonunuliwa madukani. Ng'ombe anafaa kupewa maji safi na ya kutosha.

Ng'ombe huishi ndani ya zizi. Zizi la ng'ombe linafaa kuwa safi kila wakati. Ng'ombe anahitajika kupewa matibabu ili awe na afya nzuri. Wewe unampenda mnyama gani?

---

**41.** Kulingana na ufahamu, ng'ombe anaishi wapi?
A. Zizini B. Msituni
C. Kichakani D. Mtoni

**42.** Chagua jibu ambalo ni kweli kulingana na ufahamu.
A. Ng'ombe wote wana pembe.
B. Ng'ombe wote wana nundu.
C. Ng'ombe hana faida yoyote.
D. Kuna ng'ombe ambao hawana pembe na nundu.

**43.** Chakula gani ambacho ng'ombe anaweza akatupa?
A. Nyama na maziwa.
B. Ngozi na pembe.
C. Mkoba na viatu.
D. Ngozi na mishipi.

**44.** Ufahamu unaeleza kuwa nyama huweza kuliwa na vyakula vituatavyo isipokuwa;
A. ugali B. chai
C. chapati D. wali.

**45.** Nyama na maziwa huwa na faida gani kwa binadamu?
A. Humletea pesa.
B. Huzuia magonjwa.
C. Humjengea mwili.
D. Humpa nguvu.

**46.** Mchuzi unaotokana na mifupa na nyama ya ng'ombe unafaidi sehemu gani ya mwili?
A. Ubongo B. Mifupa
C. Tumbo D. Mgongo

**47.** Ni nini ambacho hakiwezi kikaundwa kutokana na ngozi?
A. Gundi B. Viatu
C. Mkanda D. Mkoba

**48.** Ng'ombe anaweza akala nini kulingana na ufahamu?
A. Nyasi na maji
B. Maji na majani
C. Nyasi na majani
D. Chumvi na unga

**49.** Ukitaka ng'ombe wako awe na afya nzuri, unafaa kufanya nini?
A. Kumpa chakula kingi.
B. Kumpa maji mengi.
C. Kusafisha zizi lake.
D. Kumpa matibabu.

**50.** Kulingana na ufahamu, ng'ombe ni;
A. mnyama ambaye hana faida
B. mnyama mzuri
C. mnyama hatari
D. mnyama mbaya.